**MUHTASARI WA KIKAO CHA CMT KILICHOKETI TAREHE 05.11.2021 KATIKA UKUMBI MKUBWA WA MANISPAA.**

**KU/SMC/CMT/31/2021: WALIOHUDHURIA**

**A. WATAALAM**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndg. Jacob J. Mtalitinya | - | Mkurugenzi Manispaa – Mweyekiti |
| 2. Ndg. Beatrice Mushi | - | Afisa Utumishi na Utawala- Katibu |
| 3. Ndg. Afrael Manase | - | Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 4. Ndg. Kerry Mwansele | - | Kaimu Mweka Hazina |
| 5. Ndg. Robert Tarimo | - | Afisa Elimu Msingi |
| 6. Ndg. Martin Masele | - | Afisa Mazingira |
| 7. Ndg. Obeid Mwakalinga | - | Afisa Ugavi |
| 8. Ndg Andrew Zumba | - | Afisa Uchaguzi |
| 9. Ndg. Richard Mkandarasi | - | Afisa Biashara |
| 10. Ndg. Sylivester Mwenekitete | - | Afisa Elimu Sekondari |
| 11. Eng. Denis Eliakimu | - | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi |
| 12. Ndg. Deogratius Masalu | - | Mkaguzi wa Ndani |
| 13. Ndg. Janefrda Manuma | - | Afisa TEHAMA |
| 14. Dr. Sebastine Siwale | - | Mganga Mkuu |
| 15. Ndg. Salustine Shirima | - | Kaimu Afisa Kilimo |
| 16. Ndg. Victor Ndikzu | - | Afisa Mifugo |
| 17. Ndg. Fortunatus Lyapa | - | TSD |
| 18. Ndg. James Makwinya | - | Mwanasheria |

**B. SEKRETARIETI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndg. Khadija Dalasia | - | Katibu wa Vikao Manispaa |

**C. WASIOHUDHURIA**

**1. WATAALAM**

Hakuna

**KU/SMC/CMT/32/2021: KUFUNGUA KIKAO.**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao.Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote kwa kuitikia wito wa kuhudhuria Kikao. Aliwaomba wajumbe kuchangia kwa umakini na kuwa huru katika kikao hiki Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 8:30 Asubuhi.

**KU/SMC/CMT/33/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA DONDOO**

Ziliwasilishwa dondoo za kikao cha tarehe 05.11.2021 na wajumbe walizipokea kuwa ni dondoo halali za kikao.

**KU/SMC/FU/32/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 17.02.2022**

Muhtasari ulisomwa na kusahihishwa uk wa 2 kisha Mwenyekiti na Katibu wakauwekea saini Muhtasari wa tarehe 17.10.2021.

**KU/SMC/FU/32/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 17.10.2021**

Iliwasilishwa taarifa ya utekelezaji wa maazimio na wajumbe walichangia kama ifuatavyo:

Kwa Upande wa Mkandarasi wa Stendi ya Katumba azimio wajumbe walisema kuwa anatakiwa kufanya marekebisho kwa sababu mapungudfu yaliyopo yanatokana na kazi amabaztyo ameshaifanya na sio kazi mpya ambayo inasubiri fedha kutoka hazina kwani fedha zinazokuja ni kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa Stendi

**AZIMIO**

- Mapungufu yaliyopo katika Stendi ya Katumba Azimio yabainishwe na yawasilishwe katika kikao cha Morning Brief ili CMT waweze kuyajua
- Iwasilishwe taarifa ya Fedha zinazosubiriwa kutoka hazina zitafanya kazi gani katika kituo cha Mabasi cha Katumba Azimio
- Iwasilishwe Barua aliyoandikiwa Mkandarasi kwa ajili ya kufanya marekebisho katika stendi ya Katumba Azimio
- Iwasilishwe taarifa ya Mapungufu yaliyobainishwa katika ziara ya Mkuu wa Mkoa katika Stendi ya Katumba Azimio ikionesha Mangapi yametekelezwa na Mangapi hayajatekelezwa

**Hoja**

Mwenyekiti alipenda kufahamu ni kwanini Stika katika Magari hazijaanza kutumika?

**Jibu**

Afisa Biashara aliwaambia wajumbe kuwa kuanzia tarehe 07/02//2022 stika zitaanza kutumika

**AZIMIO**

Idara ya Fedha ihakikishe ifikapo tarehe 07/02/2022 stika kwa ajili ya vyombo vya usafirishaji zinaanza kutumika kama ilivyoagizwa

Kwa Upande wa Suala la kurebiesha taarifa ya Makusanyo kwenye Mfumo wajumbe walisema kuwa hakukuwa na taarifa rasmi ya maandishi ikionesha kuwa Hazina hawatambui mapato ya Mwenye Shule ya Msingi, Viwanja ya Nambogo hali iliyopelekea Mapato ya Halmashauri ya Manispaa kusomeka kuwa tumekusanya chini ya 50%

Hivyo wajumbe walisema kuwa kua haja ya kujiridhisha ni kwanini akaunti hizi hazisomi katika Mfumo wa Mapato na kama upo uwezekano wa kupata akaunti zitakazosoma kwenye mfumo basi zitumike hizo.

**AZIMIO**

- Idara ya Fedha ihakikishe inawasilisha taarifa ya mapato ambayo hayakutambulika katika taarifa ya Waziri wa Tamisemi iliyopelekea kuonesha Halmashauri imekusanya Mapato kwa 43%
- Mazungumzo yaliyofanywa na Mwekahazina na Watu wa Tamisemi kuhusu Mapato amabyo hayapo kwenye Mfumo ayaweke kwenye maandishi ili tupate majibu yao kwa njia ya maandishi
- Idara ya Fedha ihakikishe Akaunti zote ambazo hazipo kwenye Mfumo wa Mapato kama vile akaunti ya shule ya Mwenge B, Mradi wa Tofali na Viwanja inaingizwa kwenye Mfumo ili tatizo hili lisijirudie katika robo inayofuata
- Idara ya Fedha ihakikishe inafanya usuluhishi wa mapato kwenye Mfumo wa Mapato na kile kinachokusanywa kila Mwezi kabla ya Tarehe 05 uya kila Mwezi
- Mkaguzi wa Ndani awe anafanya ukaguzi kuhusu usuluhishi wa Mapato na kutoa taarifa mapema kuhusu athari zinaweza kujitokeza iwapo uslushishi hautafanyikaMwekahazina, Afisa Biashara Afisa Tehama wapeleke maelezo ya Maandishi kwanini Halmashauri imekusanya chini ya 50% kulingana na taarifa ya Waziri wakati kiuhalisia Halmashauri imekusanya kwa 53%

Kwa Upande wa Mkataba wa Mzabuni wa Taka wajumbe walisema kuwa ili Mkataba uwe Mkataba halali ni lazimabaadhi ya taratibu zifuatwe, taratibu hizo ni

- ➢ Uwepo wa Muhtasari wa Bodi ya Zabuni uliompitisha Mzabuni kuwa apewe Mkataba wa Mwaka mmoja.
- ➢ Uwepo wa Barua ya Kumtaarifu Mkurugenzi kutoka Bodi ya Zabuni.
- ➢ Uwepo wa Muhtasari wa CMT ulioridhia nyongeza ya Muda wa Mkataba

- Uwepo wa Muhtasari wa kikao cha Fedha na Uongozi ulioridhia nyongeza ya Muda wa Mktaba
- 
- Uwepo wa barua ya Tolea kwenda kwa Mzabuni kukubaliwa Nyongeza ya Muda wa Mkataba
- Kisha ndipo usainiwe Mkataba mpya wa Kuongeza Mkataba kutoka Miezi mitatu kwenda Mwaka mmoja.

Wajumbe walisema kuwa Taratibu hazikufuatwa katika sula la Kumuongeza Muda Mzabuniwa Taka.

**Jibu**

Afisa Manunuzi alisema kuwa kulikuwa na Presha kutoka nje kuhusu kumuongeza Mktaba Mzabuni huyu.

Wajumbe walisisitiza kuwa Taratibu za kumuongeza Mkataba Mzabuni wa taka hazikufuatwa hivyo Mkataba unaotambulika ni wa miezi Mitatu (03) ambao unaisha tarehe 06/02/2022

**Ushauri**

Amkaguzi wa Nadni alishauri kuwa kama Mzabuni ana mkataba wa Mwaka mmoja basi Menenjimenti ikae na kuona ni kwa namna gani tutavunja Mkataba huo kwa kupitia vipengele vilivypo kama vile uwezo mdogo wa kuzoa taka.

Mwenyekiti aliwaambia wajumbe kuwa amepokea ushauri uliotolewa na Mkaguzi wa Ndani ila anasubiri tarehe 06.02.2022 muda wa Mkataba wa kiezi mitarau utakapoisha kisha akaambiwa au Mzabuni akwasilisha Mkataba wa mwaka mmoja ndipo atakapochukua hatua stahiki.

Wajumbe walisema kuwa Bodi haikufanya kazi yake ipasavyo kwani baada ya kupokea maombi kutoka kwenye idara walitakiwa kuwasilisha maombi haya katika kiko cha CMT na Fedha na Uongozi kwa ajili ya kujadiliwa zaidi au kupata kibali.

Pia Ukiangalia Mkataba huo unaosemwa ni wa mwaka mmoja umeongezwa ukurasa mmoja wenye neno la Mwaka mmoja kisha ukasainiwa .

**AZIMIO**

Mkataba wa Mzabuni wa taka unaisha tarehe 06/02/2022 hivyo Idara ya Manunuzi na Idara ya Mazingira ihakikishe wanalisimamia hilo

Taarifa zilipokelewa

**KU/SMC/FU/33/2021: TAARIFA MBALIMBALI**

**A; MKAKATI WA UONDOAJI WA TAKA IWAPO HATAPATIKANA MZABUNI**

Afisa Mazingira aliwasilisha taarifa ya Mkakati wa Uondoaji taka iwapo tutakosa Mzabuni ambapo aliasema kuwa Hamshauri itazitumia Kata katika zoezi laUondoaji wa taka katika maeneo yetu ambapo kata zitakuwa na jukumu la Kuoa na kukusanya ushuru wa taka kwa wananchi kwa kupitiawenyeviti wa mitaa na watendaji wa mitaa.

.

**Hoja**

Wajumbe walipenda kufahamu iwapo imefanyika tathimini ya kina kujua toxo inayotozwa ya taka ina uwezo wa kuendesha shughuli za taka

**Jibu**

Afisa Manzingira aliwaambia wajumbe kuwa ushuru wa taka hautoshi kuendesea shughuli za taka

**Hoja**

Wajumbe walipenda kufahamu Halmashauri kwa siku itahitaji magari mangapi kwa ajili ya kuzoa taka

**Jibu.**

Afisa Mazingira aliwaambiwajumbe kuwa yanahitajika magari 12 kwa siku kwa ajili ya kuzolea taka kwamaana kila Kata gari moja.

Hivyo basi wajumbe walisema kuwa ni bora Halmashauri ikatumia mfumo wa kukodi magari kwa ajili ya kuondosha taka yatakayokuwa yakipita katika kata kwa Siku za Jumatatu, Jumatano na Jumosi badala ya kutumia mzabuni.
Kata zihakikishe zinapata Waazabuni wa Magari ili wapatikane wazabuni watakaotumika kubeba taka na kwa kuanzia tutakodi Magari nane (08).

**AZIMIO**

- Mgawanyo wa Mapato ya taka kuanzia tarehe 07/02/2022 itakuwa kama ifutavyo:
  Kwa kata zilizo na Mapato makubwa amabzo ni Izia, Mazwi, Katandala, majengo na Chanji watapata 40% ya Makusanyo na Halmsahauri itapata 60%.

- Na Kwa kata zilizobaki zitapata 60% na Halmashauri itapata 40% ya Makusanyo
- Kata zimepewa Zabuni ya kukusanya Mapato ya Taka na kuondoa takata hizo katika Kata zao na uandaliwe Mkataba wa Makubaliano baina ya Kata na Halmashauri
- Halmashauri itabaki na jukumu la kuondoa Maghuba katika Maeneo yaliyobainishwa
- Fedha yote inakusanywa ya Taka itaingia katika Akaunti ya Halmashauri na marejesho ya asilimia yatafanyika mara mbili kwa Mwezi kwa maana ya tarehe 15 na tarehe 25 ya kila Mwezi. Idara ya fedha ihakikishe jambo hili linafanyika kwa wakati

Idra ya Fedha , Manunuzi na TEHAMA wahakikishe ununuzi wa pOS unafanyika haraka ili POS ziweze kugawanywa kwenye Kata na watendaji waweze kukusanya Ushuru wa Taka .
Pia Kila Mlezi wa kata aahakikishe anasimamia zoezi la uondowaji wa taka zilizoko chini .

Taarifa Ilipokelewa

**B: TARIFA YA MIRADI MIKAKATI**

Kaimu Afisa Mipango takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa ya Miradi Mikakati amabyo inaweza kutekelezwa na halmashauri ya manispaa ya Sumbawanga baada ya ziara ya Kujifunza iliyofanyika Jijini Dodoma wakaona miradi kama Mradi wa Chinangali, Mradi wa Nyumba za kulala wageni , Shule za Kulipia na Kumbi za Mikutano.
Alisema kuwa miradi hii ni miradi ambayo haiitaji nguvukubwa katika usimamizi wake lakini inaweza kuingiza fedha nyingi .

- Halmashauri ianze kufanyia Kazi Maeneo ya Miradi kimkakati tuliyonayo kama Isofu na kanondo kwa kuwashirikisha wadau na pia kuanza kutenga Bajeti kwa ajili ya miradi hiyo
- Startegic Plan iboreshwe na kutengenezwa kulingana na Maono na dira tutliyonayo Halmashauri
- Halmashauri ihakikishe eneo la wauza Samaki linakamilika na Wafanyabiashara wa Samaki wanahamishiwa Mandela
- Iwasilishwe Rasimu ya Sheria ndogo ya Ushuru na Ada itakayojumuisha vyanzo vipya na kuondoa ada zenye kero kwa wananachi

Taarifa ilipokelewa

**C: TAARIFA YA MAPOKEZI NA UTEKELEZAJI WA FEDHA YA UVICO NA MATUMIZI YA FORCE ACCOUNT**

Mchumi aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha ya UVICO19 kiasi cha Tsh.1,060,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 49 na mabweni 1 kwa jili ya shule za Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Maelekezo ya fedha hizo tulitakiwa kutumia manunuzi kwa njia ya Single Source, baada ya mchakato kutofanikiwa kutokana na watenda/wazabuni kuweka gharama kubwa tofauti na gharama za fedha tulizotumiwa; wajumbe walishauri manunuzi yafanyike kwa njia ya Force Account ili kukamilisha ujenzi wa shule hizo kwa muda tuliokuwa tumepangiwa.

Taarifa ya ujenzi wa madarasa na mabweni hayo imeambatanishwa:

**KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango iliyotolewa .Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 4:10 Asubuhi.

Umesambazwa na KHADIJA DALASIA saini............. Tarehe 05/11/2022

**UMETHIBITISHWA/HAUKUTHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| .............................. | .............................. |
| Ndg. Beatrice Mushi | Ndg. Jacob J. Mtalitinya |
| Afisa Utumishi na Utawala | Mkurugenzi Manispaa |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

**TAREHE** 05/11/2022

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA**
**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA PROGRAM YA UVIKO 19**

| Na | Jina la Miradi | Kiasi Kilichopokelewa | Chanzo cha Fedha | Kiasi Kilichotumika | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa madarasa 2 shule ya Sekondari Lwiche | 40,000,000 | UVIKO-19 | 40,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 2 | Ujenzi wa darasa 1 shule ya Sekondari Kizwite | 20,000,000 | UVIKO-19 | 20,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 3 | Ujenzi wa madarasa 2 shule ya Sekondari Sumbawanga | 40,000,000 | UVIKO-19 | 40,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 4 | Ujenzi wa madarasa 3 shule ya Sekondari Mazwi | 60,000,000 | UVIKO-19 | 60,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 5 | Ujenzi wa madarasa 3 shule ya Sekondari Chanji | 60,000,000 | UVIKO-19 | 60,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 6 | Ujenzi wa madarasa 3 shule ya Sekondari Mhama | 60,000,000 | UVIKO-19 | 60,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 7 | Ujenzi wa madarasa 3 shule ya Sekondari Kichema | 60,000,000 | UVIKO-19 | 60,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 8 | Ujenzi wa madarasa 3 shule ya Sekondari Lukangao | 60,000,000 | UVIKO-19 | 60,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 9 | Ujenzi wa madarasa 3 shule ya Sekondari Itwelele | 60,000,000 | UVIKO-19 | 60,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 10 | Ujenzi wa madarasa 3 shule ya Sekondari Kalangasa | 60,000,000 | UVIKO-19 | 60,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 11 | Ujenzi wa madarasa 4 shule ya Sekondari Kanda | 80,000,000 | UVIKO-19 | 80,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 12 | Ujenzi wa madarasa 4 shule ya Sekondari Katuma | 80,000,000 | UVIKO-19 | 80,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 13 | Ujenzi wa madarasa 3 shule ya Sekondari Mbizi | 60,000,000 | UVIKO-19 | 60,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 14 | Ujenzi wa madarasa 3 shule ya Sekondari Mafulala | 60,000,000 | UVIKO-19 | 60,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 15 | Ujenzi wa madarasa 3 shule ya Sekondari Kilimani Maweni | 60,000,000 | UVIKO-19 | 60,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 16 | Ujenzi wa madarasa 2 shule ya Sekondari Ipepa | 40,000,000 | UVIKO-19 | 40,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 17 | Ujenzi wa madarasa 04 shule ya msingi shikizi Luwa (Namwele shule mpya ya msingi) | 80,000,000 | UVIKO-19 | 80,000,000 | Mradi umekamilika na unatumika |
| 18 | Ujenzi wa Bweni 01 shule ya Wanafunzi wenye mahitaji maalum ya Kizwite | 80,000,000 | UVIKO-19 | 80,000,000 | Jengo limesha ezekwa, upigaji wa lipu unaendelea. |
| | **Jumla** | **1,060,000,000** | | **1,060,000,000** | |

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 15/12/2021 KATIKA OFISI YA AFISA ELIMU MSINGI WA MANISPAA YA SUMBAWANGA.**

**WALIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Frank Mateni | - | Mwenyekiti |
| 2. | Obeid Mwakalinga | - | Katibu |
| 3. | Andrew Zumba | - | Mjumbe |
| 4. | Thadeo Maganga | - | Mjumbe |
| 5. | Robert Tarimo | - | Mjumbe |
| 6. | James Makwinya | - | Mjumbe |

**SEKRETARIETI.**

1. Neema Maliwa
2. Mussa Nginila

**AGENDA ZA KIKAO.**

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha dondoo.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao kilichopita cha Tarehe 22/10/2021.
4. kupewa taarifa ya utekelezaji wa ujenzi wa madarasa ya UVIKO 19.
5. Kupitia makadirio ya Mhandisi ya Ujenzi wa Zahati ya Mponda, Matanga na Nambogo
6. Taarifa ya mapokezi ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya kata ya Momoka .
7. Ushuru wa uzoaji taka na kupitisha mkataba wa uzoaji taka
8. Taarifa ya matengenezo na mapokezi ya magari 3

10. Yatokanayo kwenye kikao.

11. Kufunga kikao

**AGENDA NAMBA SMC/MTB/2021/2022/02. KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 4:00 Asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe wote waliohudhuria kikao, aidha aliwaomba wajumbe ushirikiano kwa kuwa bodi imepewa dhamana kubwa ya kusimamia sheria za Manunuzi yote ya Taasisi na kutoa ushauri. Pia alisisitiza wajumbe wote ni lazima kuzisoma sharia na kuzifahamu na kisha kuzifanyia kazi.

**AGENDA NAMBA SMC/MTB/2021/2022/2. KUTHIBITISHA DONDOO.**

Mwenyekiti alimkaribisha Katibu wa Bodi ya Zabuni kwa ajili ya kusoma dondoo za kikao . Baada ya kuzisoma wajumbe walikubaliana nazo na kuzithibitisha.

**AGENDA NAMBA SMC/MTB/2021/2022/03.KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 22/10/2021.**

Mwenyekiti alimkaribisha Katibu wa Bodi ya Zabuni na kusoma Muhtasari wa Kikao kilichopita cha tarehe.22/10/2021. Baada ya kusoma mwenyekiti aliwauliza wajumbe kama kuna marekebisho ,Wajumbe walisema kuna marekebisho kwenye jedwali la madarasa ya shule ya msingi yoliokuwa yamepungua na kufikia idadi ya madarasa 49 na sio 45 ya shule za sekondari pekee , na pia waliongezea fedha zilizopokelewa jumla ni 980,000,000.00 ambayo 900,000.000.00 ni kwa ajaili ya ujenzi wa madarasa na Tshs 80,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Bwini la wenye mahitaji maalumu katika shule ya Malangali. Aidha wajumbe walishauri kuwepo na nakala za kutosha ili kila mjumbe awe na nakala yake. Katibu alilipokea na kukiri mapungufu hayo.

Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti na Katibu walisaini Muhtasari huo na kuwa kumbukumbu sahihi ya Kikao.

**AGENDA NAMBA SMC/MTB/2021/2022/04. KUPEWA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UVIKO 19.**

Mwenyekiti alimruhusu katibu kutoa taarifa kwa wajumbe ya utekelezaji wa mradi wa UVIKO 19 na kuuwasilisha kwa wajumbe kwa mradi ulitekelezwa kwa njia ya Force Account na kuwaambia wajumbe kuwa mradi umekamilika kwa 97% na umebaki ukamilishaji mdogo ili kuweza kukabidhi madarasa. Mwenyekiti alihoji kama kuna la nyongeza, na wajumbe wakashauri kama kuna mradi mwingine ukitokea Mageraza asipewe miradi mingi maana amechelewesha kazi sababu ya kuwa anahamisha mafundi wake hivyo kusababisha kuchelewa kwa kazi, na pia wakashauri apewe kazi kubwa iwapo mradi upo sehemu moja.

**AGENDA NAMBA SMC/MTB/2021/2022/05. KUPITIA MAKADIRIO YA MHANDISI WA UJENZI KATIKA UJENZI WA ZAHANATI YA MATANGA, NAMBOGO NA MPONDA**

Mwenyeketi alimkaribisha katibu ili asome makadirio ya Mhandisi wa Ujenzi wa Zahanati ya Mponda, Nambongo na Kituo cha Afya Matnga. Aidha katibu alitoa taarifa ya mapokezi ya fedha kwa Zahanati ya Mponda Tshs 50,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa OPD na Maabara, Zahanati ya Nambogo Tshs 67,269,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa OPD na Maabara na Tshs 250,000,000.00 kwa kituo cha Afya Matanga kwa ajili ya ujenzi wa OPD, Maabara na kichomea taka. Aidha Katibu aligawa BOQ kwa wajumbe ili waweze kuzipitia na kutoa maoni wakati wa Katibu akiwapitisha. Aidha Mwenyekiti aliruhusu wajumbe kutoa maoni kuhusu mapitio ya BOQ, aidha wajumbe walihoji kwanini kuna utofauti wa bajeti kati ya Zahanati ya Nambogo na Mponda na wakati ramani zinafanana, pia walishauri wapate taarifa ya muhandisi ili waweze kuyapitisha makadirio hayo ya kiuhandisi. Pia wajumbe wa Bodi waliazimia kufanya Ziara ya kutemebelea Miradi hiyo ili kuweza kubaina kama kutakuwa na mabadiriko ya makadirio ya kiuhandisi, pia wajumbe walishauri mwandisi wakati anaanda BOQ aweke uhalisia wa bie au itafutwe njia mbadalaa ya kupunguza bei.

**AGENDA NAMBA SMC/MTB/2021/2022/06. TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KWA AJILI YA UJENZI WA SHULE KATIKA KATA YA CHANJI.**

Mwenyekiti alimruhusu Katibu aelezee juu ya fedha tunazozitarajia kupokea kwa ajili ya ujenzi wa shule. Aidha katibu alitoa taarifa kwa wajumbe wa Bodi matarajio ya kupokea fedha kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa shule sekondari mpya katika kata ya Chanji eneo la Momoka kiasi cha Tshs 470,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 8, jengo la utawala, Tehama pamoja na ujenzi wa vyoo ambayo itatekelezwa kwa njia ya Manunuzi ya Force Account.

**AGENDA NAMBA SMC/MTB/2021/2022/07. USHURU WA UZOAJI TAKA NA KUINGIA MKATABA WA MUDA KATI SMC NA EFO INVESTMENT**

Mwenyekiti alitoa nafasi kwa wajumbe wenye hoja mbalimbali, mjumbe alitoa mapendekezo kutoka kwa Mzabuni ya kuomba aongezewe muda maana miezi mitatu haitoshi kwa maana ameanza kwa kutumia gharama kubwa katika uendeshaji wake kwa kukodi vijiko kwa ajili ya kuzolea taka zilizo chini, pia mkataba wa miezi mitatu hawezi kuombea mkopo kwa ajili ya uendeshaji kazi na pia kilikuwa na mrudikano wa taka nyingi ambazo Manispaa ilitakiwa kuziondoa ili Mzabuni aendelee na uzoaji,

wajumbe walikubariana kuongeza muda kwa Mzabuni kwenye mkataba na Manispaa itekeleze maadhimio yake ya kutengeneza magari, Ununuzi wa POS na wajumbe walishauri apewe mkataba wa miezi 12 ikiwa miezi 6 ya mwanzi ni ya matazamio.

**AGENDA NAMBA SMC/MTB/2021/2022/08. TAARIFA YA MATENGENEZO NA MAPOKEZI YA MAGARI 3**

Mwenyeketi alimkaribisha katibu ili asome taarifa ya mapokezi na matenegenezo ya magari 3. Aidha katibu alitoa taarifa kwa wajumbe ya kupokea magari 3 ambayo ni T/Cruiser STK 4497 kutoka Hazina ambalo matengenezo yake ni Tshs 12,541,512.00, T/Cruiser SU 38503 kutoka PSSF ambalo matenegenezo yake ni Tshs 18,606,240 na Nissan Patrol SM 3880 kutoka NSSF ambalo matenegezo yake ni Tshs 11,611,200.00. Mwanyekiti aliwahoji wajumbe kama kuna maoni yoyote, Wajumbe waliomba kuona taarifa kutoka TEMESA na kukubalina kupitisha matengenezo haya kwa njia ya Circular Resolution baada ya kuona hiyo taarifa kutoka TEMESA

**AGENDA NAMBA SMC/MTB/2021/2022/09 YATOKANAYO KWENYE KIKAO**

Mwenyekiti alitoa nafasi kwa wajumbe wenye hoja mbalimbali, Wajumbe waliomba kuwe na chakula kwenye vikao vya Bodi ya Zabuni, wajumbe walikumbushia mahitaji ya shajala robo ya pili katika Halmashari na kuiomba idara ya Manunuzi kupitia kila idara kujua mahitaji na kuyapitisha mahitaji haya kwa Circular Resolution.

**AGENDA NAMBA SMC/MTB/2021/2022/10 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga Kikao mnamo saa 08:00 mchana kwa kuwashukuru Wajumbe kwa ushiriki wao, aidha alieleza kwamba sheria na taratibu zote zizingatiwe kama ushauri ulivyotolewa na Wajumbe wa kikao hicho.

**UMETHIBITISHWA/HAUJATHIBITISHWA.**

**MWENYEKITI:**

**JINA:** Frank J Maten

**SAHIHI:** ....................

**KATIBU:**

**JINA:** ASHA MILASI

**SAHIHI:** ....................

**TAREHE:** 29/3/2022